



8 Aprili 2016

Kumb. yako Na. : TP/HM/SI/A.20/MKMOVOL.II/18

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa  
Halmashauri ya Manispaa ya Singida  
S. L. P 236  
SINGIDA

**YAH: OMBI LETU LA KUBADILI MATUMIZI YA VIWANJA 28-35  
VILIVYOPO BLOCK A, ENEO LA NJUKI, MANISPAA YA SINGIDA**

Tafadhali rejea barua yako Kumb Na TP/HM/SI/A.20/MKMOVOL.II/18 ya 17 Machi 2016, inayojibu maombi yetu yahasuyo somo tajwa hapo juu.

Wakati tunashukuru kupata majibu ya maombi yetu, tunasikitika kwa kuwa majibu haya yamechukua muda mrefu sana tokea tulete maombi yetu kupitia barua yetu ya 19 Octoba 2015, na vilevile kwa kuwa maandalizi kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kufua mafuta ya alizeti yamefikia kiwango cha juu. Ni zaidi ya miezi miwili sasa mitambo yote na machine za ujenzi wa kiwanda hiki vimefika kwenye viwanja husika, ila ujenzi umeshindwa kuanza kwa kusubiri majibu ya maombi ya kubadli matumizi.

Tunasikitika zaidi pia kwa vile tumepata sehemu hiyo kutoka kwa wenyeji na kuchukua jukumu la kupimisha na hatimaye kupatiwa barua ya tozo (Offer Letter Na. SG/MLO/A/28-35 ya tarehe 15 Octoba 2015.

Kuhusu suala la kuhakikisha kuwa uendeshaji wa kiwanda unakuwa rafiki kwa mujibu wa sheria husika ya mipango miji na utunzaji wa mazingira kwenye sehemu za makazi, tunapenda kukutaarifu kuwa Baraza la Mazingira (NEMC)

---

3<sup>rd</sup> Floor, The Arcade, Mwai Kibaki Road, Mikocheni,  
P. O. Box 106242 Dar Es Salaam, Tanzania  
Tel/Fax: +255-22-2771580;



wameshakwisha tembelea sehemu husika kwa ajili ya kutafiti na kuelekeza namna ambavyo kiwanda hiki kinaweza kuendeshwa katika maeneo haya kwa mazingira rafiki. Tatizo ni kwamba ripoti yao inasubiri kwanza barua ya kukubaliwa kubadilisha matumizi ya viwanja hivyo. Tunatambua pia kuwa maeneo ya sehemu husika bado ni ya wazi na inatumika kwa ajili ya mashamba hivyo ujenzi wa kiwanda hautakuwa na usumbufu kwa watu.

Hivyo basi kwa kuzingatia kuwa mipango ya ujenzi wa kiwanda hicho umefikia kiwango cha juu na gharama kubwa zimeshatumika mpaka sasa, na kwasababu hatujui ni lini Masta Plani ya Manispaa itakamilika, tunaomba kukubaliwa kubadili matumizi ya viwanja hivyo kwa kuzingatia kuwa utekelezaji wa Sheria husika ya Mipango miji ya mazingira rafiki kwenye makazi itatekelezwa kwa kufuata maelekezo ya NEMC.

Kwa kuzingatia maelezo haya, tunapenda kufikiriwa tena ombi letu la kubadilishiwa matumizi ya viwanja hivyo kwa ajili ya kujenga kiwanda hiki ambacho tunatumaini kitaongeza tija kubwa kwa mkoa wa Singida na hivyo kwenda sambamba na sera rafiki ya kukuza uchumi wa viwanda chini ya serikali ya awamu ya tano.

Tunatanguliza shukrani zetu kwako na tunategemea barua hii itajibiwa kwa wakati muafaka.

Wako mtiifu,

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Emmanuel Nagunwa".

**Emmanuel Nagunwa**  
**Mkurugenzi**

---

3<sup>rd</sup> Floor, The Arcade, Mwai Kibaki Road, Mikocheni,  
P. O. Box 106242 Dar Es Salaam, Tanzania  
Tel/Fax: +255-22-2771580;